washington healthplanfinder

click. compare. covered.

# Mambo Muhimu kuhusu Bima ya Afya

KILA KITU UNACHOPASWA KUJUA KUHUSU KUWA NA BIMA



# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| **4** | *Washington Healthplanfinder* |
| **5** | Maneno Muhimu |
| **6-7** | Mambo Muhimu kuhusu Bima ya Afya |
| **8** | Manufaa |
| **9** | Msaada wa kifedha |
| **10** | Washington Apple Health (Medicaid) |
| **11** | Kuchagua Bima ya Afya |
| **12-14** | Cascade Care |
| **15-16** | Wakati wa Kutuma Maombi |
| **17** | Orodha-Kaguzi ya Kutumia |
| **18-23** | Jinsi ya Kutuma Maombi |
| **23** | Tufuate! |

# *Washington Healthplanfinder*

## *Washington Healthplanfinder* ni Nini?

*Washington Healthplanfinder* ni sehemu ya kununua bima ya afya mtandaoni katika jimbo la Washington. Watu wa Washington wanaweza kupata bima ya afya inayowafaa kupitia sisi.

*Washington Healthplanfinder* inatoa bima na mapunguzo yasiyopatikana kwingine kokote. Bima za Cascade Care zinatoa huduma zaidi na mapunguzo kuliko bima nyingine nyingi. Programu za mapunguzo kama punguzo la kodi zinaweza kushusha gharama ya ada yako ya bima. Huwezi kupata manufaa haya kwingine kokote.

## Natumiaje *Washington Healthplanfinder*?

Ni rahisi kutuma maombi ya bima ya afya kupitia *Washington Healthplanfinder*. Unaweza kujisajili na kununua kwenye wahealthplanfinder.org, app ya WAPlanfinder au kwa njia ya simu.

Pakua App
**WAPlanfinder**

Tembelea Tovuti Yetu
**wahealthplanfinder.org**

## Una Maswali? Wasiliana na Usaidizi kwa Wateja.

Kituo chetu cha Usaidizi kwa Wateja kinatoa usaidizi katika lugha zaidi ya 200.

Simu: **1-855-923-4633**
TTY: **1-855-627-9604**

# Maneno Muhimu

Maneno Haya ni Msingi wa Kuelewa Bima Yako Ya Afya.

### Ada ya Bima

Ada ya bima ni kiasi unacholipa kila mwezi kwa ajili ya bima yako ya afya. Unapaswa kulipa ada yako ya bima hata kama hutumii huduma zozote za matibabu ya afya.

### Gharama Shirikishi

Gharama shirikishi ni kiasi cha gharama za matibabu ya afya unacholipa. Neno hili linajumuisha makato, bima shirikishi na malipo shirikishi.

### Makato

Makato yako ni kiasi unachopaswa kulipia matibabu kabla ya bima yako kuanza kushiriki gharama. Kiasi cha makato yako kinaanza upya mwanzoni mwa kila mwaka.

### Malipo Shirikishi

Malipo shirikishi ni kiasi unacholipa kwa ajili ya huduma ya afya inayolipiwa na bima yako. Malipo yako shirikishi yanapaswa kulipwa ukipokea huduma.

### Bima Shirikishi

Bima Shirikishi ni sehemu yako ya gharama ya huduma inayolipiwa na bima ya afya. Utaanza kulipa bima shirikishi baada ya kulipia makato ya bima yako ya afya.

### Kutoka Mfukoni

Gharama za kutoka mfukoni ni kile unacholipa kwa ajili ya huduma za afya. Inaweza kujumuisha makato, bima shirikishi na malipo shirikishi. Kiasi chochote kisicholipiwa na bima yako ni gharama ya kutoka mfukoni.

### Mtandao

Mtandao ni orodha ya watoa huduma wanaokubaliwa na bima yako ya afya. Watoa huduma wa ndani ya mtandao wameidhinishwa na bima yako ya afya. Watoa huduma wa nje ya mtandao hawajaidhinishwa na bima yako ya afya.

# Mambo Muhimu kuhusu Bima ya Afya

### Bima ya Afya ni Nini?

Unanunua bima ya afya kila mwaka ikitokea wewe au familia yako mnahitaji matibabu ya afya. Kampuni ya bima yako inalipa sehemu ya gharama ya matibabu ya afya ukiwa na bima ya afya.

### Kwa Nini Nahitaji Bima ya Afya?

Hata watu wenye afya njema wanatumia mfumo wa matibabu ya afya. Kuwa na bima ya afya kunakuhakikishia gharama nafuu za matibabu ya afya unapozihitaji. Unaweza kupata matibabu ya kinga ili udumu mwenye afya njema. Unaweza kupata matibabu kwa haraka kama unaumwa. Bima ya afya inatoa njia nafuu ya kupata huduma za matibabu wakati unapozihitaji.



**Bima ya Afya kwa Siku za Usoni**

Hujui lini utahitaji kwenda kuonana na daktari. Kuwa na bima ya afya kunapa uhakia wa kumudu kupata huduma za matibabu unapozihitaji.

Hata kama una afya njema, bima inakusaidia udumu na afya njema.



**Wekeza katika Afya Yako**

Gharama za matibabu ya afya zinaweza kuwa aghali bila bima ya afya. Ziara za mara kwa mara hospitalini huongezeka kwa haraka. Gharama ya matibabu ya majeraha ya dharura au ugonjwa mkubwa inaweza kumaliza akiba yako.

Unaweza kupata punguzo kubwa katika siku za usoni kwa kulipa kidogo kwenye bima ya afya hivi leo.

## Sheria ya Matibabu Nafuu ni Nini?

Baada ya kupitishwa sheria ya Affordable Care Act, jimbo la Washington liliunda *Washington Healthplanfinder*. Lengo la Sheria hii ni kufanya huduma ya afya iwe nafuu. Watu wengi sasa wanaweza kupata bima ya afya kwa kiasi kidogo au bila gharama yoyote. Hali yako inaweza kukupa ustahiki wa Washington Apple Health (Medicaid) au manufaa ambayo hupunguza kiasi unacholipia bima.

Unaweza kutuma maombi ya bima ya bila malipo au ya gharama nafuu kwenye wahealthplanfinder.org na app ya WAPlanfinder.

## Vipi Kama Nisipopata Bima ya Afya?

Utalipa gharama kamili ya matibabu ya afya bila bima ya afya. Dawa ya mafua inaweza kugharimu $50. Kulazwa siku tatu hospitali kunagharimu makumi ya maelfu. Matibabu ya saratani yanaweza kufikia mamia ya maelfu.

Unaweza pia kupigwa faini ya kodi kama huna bima. Katika Washington, unapata bima moja kwa kila mtu katika kaya yako.

## Matibabu yana Gharama Gani?

Haya ni baadhi ya matibabu ya kawaida na gharama zake. Bima yako inaweza kushiriki gharama kama hizi na wewe.

| MATIBABU | GHARAMA |
|---|---|
| Upasuaji wa Moyo | $78,585 |
| Eksirei ya Matiti (mammogram) | $263 |
| Upasuaji wa Uti wa Mgongo | $13,255 |
| Uchunguzi wa Utumbo mpana kwa kifaa Maalum | $1,484 |
| Kujifungua kwa Upasuaji | $18,098 |
| Kupata Matibabu ya Haraka | $181 |
| Uchunguzi wa Afya (kwa vijana) | $117 |
| Kupelekwa Chumba cha Dharura | $579 |

# Manufaa

### Bima ya Afya Inalipia Nini?

Bima zote za afya zinakupa manufaa haya kumi muhimu ya kiafya. Baadhi ya bima, kama bima za Cascade Care zinakupa zaidi.

**Manufaa Muhimu ya Kiafya**

- Kumwona daktari na kulazwa hospitali
- Kupelekwa Chumba cha Dharura
- Matibabu ya ujauzito
- Huduma za afya ya akili na matibabu ya matumizi ya dawa za kulevya
- Dawa za kuandikiwa na daktari
- Uangalizi wa majeraha
- Vipimo vya maabara
- Huduma za Kinga (Preventative Services)
- Matibabu ya maradhi sugu
- Matibabu ya watoto

#### Cascade Care

Unaweza kupata huduma na mapunguzo zaidi ukiwa na bima ya Cascade Care.

#### Hakuna Kukataliwa

Hutakataliwa kupewa bima kutokana na maradhi ya sasa uliyonayo.

#### Matibabu ya Kinga Bila Malipo

Huduma kama uchunguzi wa kiafya na chanjo zinalipiwa kikamilifu.

#### Ubora wa Matibabu

Bima nyingi za afya zinatoa ubora wa hali ya juu zaidi wa matibabu kuliko unayopata kama huna bima.

# Msaada wa kifedha

### Punguzo la Kodi ni Nini?

Punguzo la kodi linashusha kiasi unacholipia bima yako ya afya kila mwezi. Hii inalipwa na serikali na inapunguzwa kwenye ada yako ya bima ya afya. Punguzo la kodi linapatikana tu kupitia *Washington Healthplanfinder*.

### Nani Anaweza Kupata Punguzo la Kodi?

Kiasi cha punguzo la kodi unachopata kinategemea na kipato chako na ukubwa wa kaya yako. Kadri kipato cha kaya yako kilivyo kidogo zaidi, ndivyo unavyostahiki punguzo zaidi la kodi. Kiasi hiki kinakokotolewa wakati unapojiandikisha. Unaweza kustahiki punguzo la kodi ikiwa mambo haya ni kweli:

- Hustahiki Washington Apple Health (Medicaid) au Medicare.
- Huna bima inayotolewa na ajira yako au kupitia programu nyingine ya serikali.
- Wewe ni raia wa Marekani au mkazi halali wa Marekani na unaishi Washington.
- Kama una ndoa, hulipi Kodi Inayolipwa Tofauti kwa Wanandoa (Married Filing Separately).

### Cascade Care Savings ni Nini?

Programu ya Cascade Care Savings inashusha gharama ya ada yako ya bima ya afya. Ukiwa na ustahiki, jimbo litalipa sehemu ya ada yako ya bima.

### Nani Anaweza Kupata Cascade Care Savings?

Unaweza kustahiki kupata Cascade Care Savings ikiwa mambo haya ni kweli:

- Kipato chako ni pungufu ya 250% ya Kiwango cha Umaskini cha Serikali Kuu.
- Hustahiki Washington Apple Health (Medicaid) au Medicare.
- Una bima ya ngazi ya Fedha au Dhahabu ya Cascade Care.
- Ikiwa unastahiki punguzo la kodi, umekubali kiasi kamili unachoweza kupata.

# Washington Apple Health (Medicaid)

## Apple Healthni Nini?

Apple Health ni jina la Medicaid katika jimbo la Washington. Inalipia manufaa yote muhimu ya kiafya. Watu wengi wanaweza kupata Apple Health bila gharama yoyote. Baadhi wanaweza kulazimika kulipa ada ya kila mwezi.

Unaweza kutuma maombi ya Apple Health wakati wowote kupitia *Washington Healthplanfinder*.

## Nani Anaweza Kupata Apple Health?

Unaweza kupata Apple Health ikiwa mambo haya matatu ni kweli. Unda akaunti au ingia Washington Healthplanfinder ikiwa hujui kama una ustahiki.


- Kipato chako ni chini ya 138% ya Kiwango cha Umaskini cha Serikali Kuu.
- Wewe ni raia wa Marekani au umeishi kihalali Marekani kwa miaka mitano.
- Una miaka chini ya 65.

# Kuchagua Bima ya Afya

### Usichanganyikiwe. Kupata Bima Sahihi ni Jambo Rahisi.

Kuna mengi ya kutafakari wakati wa kuchagua bima ya afya. Unaweza kustahiki bima nyingi, lakini huna uhakika ipi ni bora kwa mahitaji yako. Bima tofauti zinatoa manufaa tofauti. Bima za Cascade Care zinatumia muundo wa ushiriki wa kawaida wa gharama kutoa manufaa bora kwa kila ngazi ya bima.

Maswali hapo chini yanaweza kukuongoza katika bima sahihi ya afya.




- **Naweza kulipa kiasi gani kwa mwezi?**
  Ada ya kila mwezi inatofautiana kati ya bima za afya.
- **Napaswa kuchangua daktari mkuu wa matibabu?**
  Baadhi ya bima zinakuchagulia mmoja.
- **Daktari wangu wa sasa yupo katika mtandao wa bima husika?**
  Hakikisha daktari wako wa sasa yupo katika mtandao.
- **Nahitaji rufaa ya maandishi kumwona mtaalamu?**
  Baadhi ya bima zinahitaji rufaa za maandishi.
- **Kubadili madaktari ni rahisi kiasi gani?**
  Unaweza kulazimika kubadili madaktari katika siku za usoni.
- **Kuna makato?**
  Lazima ulipie makato yako kabla ya bima yako kushiriki gharama.
- **Gharama za kutoka mfukoni ni zipi kwa bima hii?**
  Gharama za kutoka mfukoni zinaongezwa na ziara za mara kwa mara.
- **Bima hii inashughulikiaje kupelekewa Chumba cha Dharura?**
  Fahamu cha kufanya wakati wa dharura.
- **Unategemea gharama zozote kubwa za matibabu mwaka ujao?**
  Unaweza kuhitaji bima zaidi ikiwa unategemea mtoto au gharama nyingine kubwa.

# Cascade Care

## Bima za Cascade Care ni Nini?

Bima za Cascade Care ni aina ya Qualified Health Plan inayopatikana kupitia *Washington Healthplanfinder*. Zinakupa manufaa muhimu ya kiafya na kutoa huduma na mapunguzo zaidi kuliko bima nyingi.

Kuna aina mbili za bima za Cascade Care: Bima za Cascade na bima za Cascade Select. Bima za Cascade Select zina viwango vya juu zaidi vya kufikiwa. Zinatoa ubora na thamani zaidi kuliko bima nyingine.

## Kwa nini Nichague Bima ya Cascade Care?

Bima za Cascade Care zinakupa zaidi kwa gharama nafuu. Zinakupa huduma zaidi kuliko bima nyingi kabla ya kulazimika kulipia makato yako. Hii inajumuisha matibabu ya msingi, huduma za afya ya akili, dawa za kawaida na mengineyo.

Pia unapata punguzo la gharama za kutoka mfukoni. Kwa wastani, makato yako yanapata punguzo la $1,000 ukichagua bima ya Cascade Care.

## Bima za Cascade Care Zinafanyaje Kazi?

Bima za Cascade Care zinatumia muundo wa ushiriki wa kawaida wa gharama. Hii inamaanisha mambo kadhaa. Kwanza, gharama za kutoka mfukoni zinabaki vile vile kati ya makampuni ya bima. Bima zote za Cascade Care katika kila ngazi zinakuwa na mfanano wa makato, malipo shirikishi na bima shirikishi.

Pili, bima za Cascade Care zinalipia huduma zile zile. Zinalipia huduma zile zile kabla ya kulipia makato yako. Unaweza kuwa na uhakika kwamba umepata bima bora kabisa.

## Machaguo Zaidi. Thamani Zaidi.

Bima za Cascade na Cascade Select zinakupa machaguo zaidi na thamani zaidi. Muundo wao wa ushiriki wa kawaida wa gharama unahakikisha unapata bima bora iwezekanavyo.

Bima za Cascade Care zinapatikana tu kupitia *Washington Healthplanfinder*. Ingia kwenye akaunti yako kuona kama una ustahiki.



## Bima Zinazopatikana katika *Washington Healthplanfinder*

| | Bima zisizo za Cascade | Bima za Cascade | Bima za Cascade Select |
|---|---|---|---|
| Kustahiki punguzo la kodi | ✓ | ✓ | ✓ |
| Unastahiki Cascade Care Savings | | ✓ | ✓ |
| Bima Stahiki ya Afya (lazima kufikia viwango vya ubora) | ✓ | ✓ | ✓ |
| Inalipia mafao yote kumi muhimu ya afya | ✓ | ✓ | ✓ |
| Gharama Shirikishi Zilizosanifishwa (bima zina makato yale yale, malipo shirikishi yale yale na bima shirikishi ile ile) | | ✓ | ✓ |
| Inalipia matibabu ya msingi, matibabu ya haraka, matibabu ya afya ya akili, dawa za kawaida na mengineyo kabla ya kulipia makato | | ✓ | ✓ |
| Zinapatikana tu katika *Washington Healthplanfinder* | | ✓ | ✓ |
| Zinapatikana katika kila wilaya ya Washingston | ✓ | ✓ | |

# Wakati wa Kutuma Maombi

## Naweza Kutuma Maombi ya Bima ya Afya Wakati Gani?

Unaweza kutuma maombi ya bima ya afya kipindi cha uandikishaji. Kipindi cha uandikishaji ni wakati wa kununua Qualified Health Plans na Qualified Dental Plans kupitia *Washington Healthplanfinder*. Kinaanza Novemba 1 kila mwaka.

## Vipi Kama Nahitaji Bima Kabla ya Kipindi cha Uandikishaji?

Baadhi ya mabadiliko ya kimaisha yanakuwezesha kujiunga na bima ya afya wakati wowote wa mwaka. Hii inajulikana kama uandikishaji maalum. Unaweza kutuma maombi ya uandishaji maalum hadi siku 60 baada ya kutokea kwa tukio la kimaisha lenye ustahiki.

**Matukio ya Kimaisha Yenye Ustahiki**

- Ndoa
- Kuishi kinyumba
- Kujifungua
- Kuasili au kulea watoto
- Kustaafu mapema
- Kupoteza tegemezi au hali ya utegemezi kutokana na kifo, talaka au utengano halali kisheria.
- Badiliko la kipato
- Kupoteza bima nyingine ya afya
- Kupoteza bima ya bila malipo ya COBRA
- Kuhamia Washington
- Kuhamia nchi mpya
- Badiliko la uraia au hali ya ukazi halali kisheria
- Kuachiliwa huru kutoka gerezani
- Kupokea amri ya mahakama (ikiwemo matunzo ya watoto)

## Kaya zenye Kipato cha Chini

Kaya zenye kipato cha chini zinaweza kutuma maombi ya uandikishaji maalum wakati wowote. Si lazima kuwe na tukio la kimaisha lenye ustahiki. Lazima uwe chini ya 250% ya Kiwango cha Umaskini cha Serikali Kuu ili kupata manufaa haya.

## Watu wa AI/AN na Makabila

Sheria za uandikishaji hazihusiki kwa watu wa makabila na wadau wa Alaska Native Corporation. Unaweza kujiandikisha wakati wowote wa mwaka. Unaweza pia kuamua kubadili bima yako mara moja kwa mwezi.



# Orodha-Kaguzi ya Kutumia

## Nahitaji Nini ili Kutuma Maombi?

*Washington Healthplanfinder* inahitaji baadhi ya taarifa zako za msingi unapoomba bima ya afya. Tumia orodha-kaguzi hapo chini kuhakikisha unacho kinachohitajika.

- ☑ **Majina Halali na Tarehe za Kuzaliwa**
  Andaa jina halali na tarehe ya kuzaliwa ya kila mtu anayetuma maombi ya bima.
- ☑ **Nambari ya Huduma za Kijamii (SSN)**
  Andaa nambari ya huduma za kijamii ya kila mtu anayeomba bima kama wanayo. Unaweza kuomba hata kama huna.
- ☑ **Hali ya Kutokuwa Raia**
  Tunaweza kuhitaji kujua hali yako ikiwa wewe si raia. Wewe au wanafamilia wako mnaweza kupata bima ikiwa si raia.
- ☑ **Hali ya Kipato na Ulipaji wa Kodi**
  Andaa taarifa yoyote iliyopo ya kipato cha kila mtu anayetuma maombi. Hii inaweza kujumuisha fomu za W-2 na taarifa za ulipaji kodi.
- ☑ **Maelezo ya Bima Nyingine**
  Unaweza kuwa na chaguzi nyingine za bima ya afya, kama vile Medicare, Tri-Care au bima inayotolewa kazini. Andaa taarifa hii wakati wa kutuma maombi.

# Jinsi ya Kutuma Maombi

### Nina Kila Kitu Kinachohitajika! Nifanyeje?

Unaweza kutuma maombi ya bima katika wahealthplanfinder.org, kupitia app ya WAPlanfinder au kwa njia ya simu.

**Jisajili Mtandaoni kupitia wahealthplanfinder.org**

Unda akaunti, nunua bima za afya na pata taarifa muhimu kupitia wahealthplanfinder.org.

**Wasiliana Nasi kupitia 1-855-923-4633**

Usaidizi kwa Wateja unapatikana kwa njia ya simu kuanzia 7:30 a.m. hadi 5:30 p.m. Jumatatu hadi Ijumaa.

**Pakua app ya WAPlanfinder**

App yetu ya simu ya kiganjani inapatikana katika Apple App Store na Google Play.

### Bofya. Linganisha. Pata Bima.

Ni rahisi kupata bima sahihi kwa mahitaji yako kupitia *Washington Healthplanfinder*. Iwe unatumia wahealthplanfinder.org au app ya WAPlanfinder, fuata hatua hizi rahisi.

1 **Nunua na linganisha.** Andika umri wako, matumizi ya tumbaku na makadirio ya kipato. Utaona orodha ya bima za afya unazoweza kupata na ada zake.

2 **Tuma Maombi.** Weka taarifa zaidi, kama hali ya ulipaji kodi na vyanzo vya kipato. Hii itakuonesha kama unastahiki msaada wa kifedha, Washington Apple Health (Medicaid) au Qualified Health Plan.

3 **Chagua bima.** Unaweza kuwa na machaguo mengi kulingana na hali yako. Chagua bima bora kwako na kwa mahitaji ya familia yako.

4 **Pata bima.** Ukithibitisha bima yako ya afya uliyochagua, utakuwa umepata bima. Lipa bili ya ada yako ya kwanza ukiipata ili kuanza kutumia bima. Kampuni uliyochagua itakupatia kadi ya bima.

### Pata Usaidizi wa Maombi Yako

Tunashirikiana na wataalamu kutoka sehemu mbalimbali za jimbo ambao wanaweza kukuongoza kwenye mchakato wa kujisajili. Wataalamu hawa wanajulikana kama mawakala. Watu hawa wanaweza kujibu maswali yako kuhusu bima za afya au jinsi ya kujiandikisha. Wanaweza pia kukwambia kama una ustahiki wa msaada wa kifedha.

Usaidizi kutoka kwa mawakala kwa kawaida hauna gharama yoyote. Watafute katika eneo lako kupitia wahealthplanfinder.org au app ya WAPlanfinder.

## Vituo vya Uandikishaji vyenye Mawakala katika Miji

**Bellingham**
Rice Insurance
1400 Broadway Street, Bellingham, WA 98225
*Simu:* 1-360-734-1161
*Barua pepe:* keith@riceinsurance.com

**Everett**
Health Insurance Solutions NW, LLC
7003 Evergreen Way, Suite B, Everett, WA 98203
*Simu:* 1-425-252-5105
*Barua pepe:* neil@his-nw.com

**Federal Way**
Public Health Seattle & King County
1640 S 318th Place, Federal Way, WA 98003
*Simu:* 1-800-756-5437
*Barua pepe:* chap@kingcounty.gov

**Kennewick**
Advisor Health Benefits Group
1446 Spaulding Ave, Suite 302, Richland, WA 99352
*Simu:* 1-509-524-9611
*Barua pepe:* kevin@advisorhealthbenefits.com

**Seattle**
Financial Designs
2723 California Avenue SW, Seattle, WA 98116
*Simu:* 1-425-392-7390
*Barua pepe:* cmcclure@financialdesignsinsurance.com

**Spokane**
Better Health Together Enrollment Center
157 S Howard, Ste 102, Spokane, WA 99201
*Simu:* 1-509-370-5605
*Barua pepe:* bhtnavigatorstaff@BetterHealthTogether.org
*Tovuti:* www.betterhealthtogether.org/navigators

**Tacoma**
FND Insurance & Financial Services, LLC
5515 Steilacoom Blvd SW, Suite 122, Lakewood, WA 98499
*Simu:* 1-253-302-5579
*Barua pepe:* teamfnd@fndinsurance.com

**Vancouver**
Applied Team Insurance
8513 NE Hazel Dell Avenue, Suite 101, Vancouver, WA 98665
*Simu:* 1-360-726-6092
*Barua pepe:* marlena@appliedteamins.com

**Wenatchee**
Suzie Health Insurance
413 N Mission Street, Wenatchee, WA 98801
*Simu:* 1-509-295-9055
*Barua pepe:* info@wahbroker.org

**Yakima**
Yakima Neighborhood Health Services
610 Yakima East Avenue, Yakima, WA 98901
*Simu:* 1-509-853-2377
*Barua pepe:* navigators@ynhs.org

## Enrollment Centers with Navigators by County

**Wilaya ya Adams, Ferry, Lincoln, Pend Oreille, Spokane, Stevens au Whitman**
Better Health Together
*Simu:* 1-509-381-5573
*Barua pepe:* bhtnavigatorstaff@BetterHealthTogether.org
*Tovuti:* www.betterhealthtogether.org/navigators

**Wilaya ya King, Clallam au Jefferson**
Public Health Seattle & King County
*Simu:* 1-800-756-5437
*Barua pepe:* chap@kingcounty.gov

**Wilaya ya King, Pierce, Snohomish au Thurston**
Korean Women's Association
*Simu:* 253-535-4202
*Tovuti:* www.kwacares.org

**Wilaya ya Chelan, Douglas, Grant au Okanogan**
Confluence Health/Wenatchee Valley Hospital
*Simu:* 1-509-433-3383
*Barua pepe:* sm_ch_lead_org@confluencehealth.org

**Wilaya ya Kitsap**
Peninsula Community Health Services
*Simu:* 1-360-377-3776
*Barua pepe:* eligibility@pchsweb.org

**Wilaya ya Clark, Cowlitz, Grays Harbor, Klickitat, Lewis, Mason, Pacific, Pierce, Thurston, Snohomish, Skagit, Skamania, Wahkiakum au Whatcom**
Sea Mar Community Health Centers
*Simu:* 1-855-289-4503
*Barua pepe:* seamaripa@seamarchc.org

**Wilaya ya Asotin, Benton, Columbia, Franklin, Garfield au Walla Walla**
Tri-Cities Community Health
*Simu:* 1-509-543-1952
*Barua pepe:* enrollmentHBE@mytcch.org
*Tovuti:* www.mytcch.org

---

**Wilaya ya Kittitas au Yakima**
Yakima Neighborhood Health Services
*Simu:* 1-509-853-2377
*Barua pepe:* navigators@ynhs.org




# Tufuate!

Tunashirikisha taarifa muhimu na habari mpya za uandikishaji kwenye chaneli hizi za mitandao ya kijamii.

- Washington Healthplanfinder
- waplanfinder
- waplanfinder

washington
healthplanfinder
click. compare. covered.

wahealthplanfinder.org
1-855-WAFINDER | 1-855-923-4633